



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**TAKWIMU ZA WAFUNGWA NA MAHABUSU
TANZANIA BARA MWAKA
2013 NA 2014**



**Jeshi la Magereza Tanzania Bara
Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi
Dar es Salaam**



**Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Wizara ya Fedha
Dar es Salaam**

YALIYOMO

Orodha ya Majedwali	v
Orodha ya Michoro	viii
Majedwali Ambatanisho	ix
Maana ya Vifupisho	xi
Dibaji	xii
Shukrani	xiii
Muhtasari	xiv
SURA YA KWANZA.....	1
USULI	1
1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Jiografia na Utawala.....	1
1.2 Jeshi la Magereza	2
1.2.1 Majukumu ya Jeshi la Magereza.....	2
1.2.2 Takwimu za Jeshi la Magereza	2
1.2.3 Kitengo cha Takwimu cha Jeshi la Magereza.....	3
SURA YA PILI.....	4
HALI YA MAGEREZA NCHINI	4
2.0 Utangulizi.....	4
2.1 Muhtasari wa Hali ya Magereza	4
SURA YA TATU	5
TAKWIMU ZA WAHALIFU WALIOKUWEPO MAGEREZANI	

5

3.0	Utangulizi.....	5
3.1	Takwimu za Wahalifu kwa Mkoa na Jinsi.....	5
3.2	Wafungwa Waliobaki Magerezani kwa Mkoa na Umri	7
3.3	Wafungwa Waliobaki Magerezani kwa Mkoa, Jinsi na Tabia	9
3.4	Wafungwa wa Adhabu ya Kifo Waliobaki Magerezani kwa Mkoa na Hali ya Rufaa.	11
3.5	Wafungwa Watu Wazima na Vijana Waliobaki Magerezani kwa Jinsi na Aina ya Kosa	12
3.6	Wafungwa Waliokuwepo Magerezani kwa Jinsi, Aina ya Kosa na Urefu wa Kifungo.....	14
3.7	Mahabusu Watu Wazima na Vijana Waliokuwepo Magerezani Kusubiri Kesi kwa Jinsi, Aina ya Kosa na Muda Waliokaa Gerezani.....	16
3.8	Wahalifu Wenye Ugonjwa wa Akili Waliobaki Magerezani	20
3.9	Wahalifu wanawake wajawazito na wenye watoto.....	20
3.10	Wafungwa Wasio Raia Waliokuwepo Magerezani, kwa Jinsi, Aina ya Kosa na Nchi Walizotoka	22
3.11	Mahabusu Wasio Raia Waliokuwepo Magerezani kwa Aina ya Kosa na Jinsi.....	24

SURA YA NNE.....26

WAHALIFU WALIOPokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani 26

4.0	Utangulizi.....	26
4.1	Wahalifu Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani, kwa Jinsi na Mkoa	26
4.2	Wafungwa Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Umri, Jinsi na Mkoa	29
4.3	Wafungwa Warudiaji Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi na Mkoa	32
4.4	Wafungwa Watu Wazima Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi, Aina ya Kosa na Urefu wa Kifungo	34
4.5	Wafungwa Vijana Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi, Aina ya kosa na Urefu wa Kifungo	37
4.6	Wafungwa Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Kushindwa Kulipa Faini kwa Mkoa na Urefu wa Vifungo	40
4.7	Wafungwa Wagonjwa wa Akili Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi na Mkoa	41
4.8	Wahalifu Wanawake Wajawazito na Wenye Watoto Waliopokelewa Magerezani Toka Mahakamani kwa Aina ya Kosa	41
4.9	Mahabusu Watu Wazima Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi, Aina ya kosa na Muda wa Kusubiri Hukumu.....	42

4.10	Mahabusu Vijana Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi, Aina ya kosa na Muda wa Kusubiri Hukumu.....	44
4.11	Wafungwa Wasio Raia Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi na Nchi Walizotoka.....	45
4.12	Mahabusu Wasio Raia Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi na Nchi Wanazotoka	46
SURA YA TANO.....		49
WAHALIFU WALIOHAMISHWA KUTOKA GEREZA MOJA KWENDA JINGINE		49
5.0	Utangulizi.....	49
5.1	Wahalifu Waliohamishwa kwa Jinsi na Mkoa.....	49
5.2	Wafungwa wenye Ugonjwa wa Akili kwa Jinsi na Mkoa Waliopokelewa kutoka Magereza Mengine.....	51
SURA YA SITA.....		52
WAHALIFU WALIOTOKA MAGEREZANI		52
6.0	Utangulizi.....	52
6.1	Wahalifu Waliotoka Magerezani Mwaka 2013 na 2014	52
6.2	Wafungwa Walioachiwa kwenda Kutumikia Kifungo cha Nje kwa Jinsi na Mkoa.....	55
6.3	Wafungwa Walioachiwa Baada ya Kulipa Faini kwa Urefu wa Kifungo na Mkoa	58
6.4	Wahalifu Waliotoroka Magerezani Chini ya Ulinzi Halali Magerezani kwa Jinsi na Mkoa	59
6.5	Wahalifu Waliofariki Magerezani kwa Jinsi na Mkoa	60
SURA YA SABA		62
WAHALIFU WALIOPEWA ADHABU KWA MAKOSA YA UTOVU WA NIDHAMU WAKIWA MAGEREZANI		62
7.0	Utangulizi.....	62
7.1	Wahalifu Waliopewa Adhabu Magerezani kwa Aina ya Adhabu na Mkoa	62
SURA YA NANE.....		65
MAHABUSU WALIOHUKUMIWA ADHABU ZA VIFUNGO WAKIWA MAGEREZANI		65
8.0	Utangulizi.....	65
8.1	Mahabusu Waliohukumiwa Wakiwa Magerezani kwa Jinsi na Mkoa	65
SURA YA TISA.....		67
HITIMISHO		67
9.0	Utangulizi.....	67

9.1 Hitimisho.....67

Orodha ya Majedwali

Jedwali 3.1:	Idadi ya Wahalifu Waliobaki Magerezani kwa Mkoa na Jinsi, Tanzania Bara, 2013 na 2014.....	6
Jedwali 3.2:	Idadi ya Wafungwa Waliobaki Magerezani kwa Mkoa na Umri, Tanzania Bara, 2013 na 2014.....	8
Jedwali 3.3:	Idadi ya Wafungwa Waliobaki Magerezani kwa Mkoa, Jinsi na Tabia, Tanzania Bara, 2013 na 2014	10
Jedwali 3.4:	Idadi ya wafungwa wa Adhabu ya Kifo Waliobaki Magerezani kwa Mkoa na Hali ya Rufaa, Tanzania Bara, 2013 na 2014	11
Jedwali 3.5:	Idadi ya Wafungwa Watu Wazima na Vijana Waliobaki Magerezani kwa Jinsi na Aina ya Kosa, Tanzania Bara, 2013 na 2014.....	13
Jedwali 3.6:	Idadi ya Wafungwa Watu Wazima Waliokuwepo Magerezani kwa Jinsi na Urefu wa Kifungo, Tanzania Bara, 2013 na 2014	14
Jedwali 3.7:	Idadi ya Mahabusu Waliokuwepo Magerezani kwa Jinsi na Aina ya Kosa, Tanzania Bara, 2013 na 2014	16
Jedwali 3.8	Idadi ya Wahalifu Wanawake Wajawazito na Wenye Watoto kwa Aina ya Kosa, Tanzania Bara, 2013 na 2014	21
Jedwali 3.9:	Idadi ya Wafungwa Wasio Raia Waliokuwepo Magerezani kwa Jinsi na Aina ya Kosa Tanzania Bara, 2013 na 2014	22
Jedwali 3.10:	Idadi ya .Mahabusu Wasio Raia Waliokuwepo Magerezani kwa Aina ya Kosa na Jinsi Tanzania Bara, 2013 na 2014	24
Jedwali 3.11:	Idaddi ya Mahabusu Wasio Raia Waliokuwepo Magerezani kwa Jinsi na Nchi Walizotoka, Tanzania Bara, 2013 na 2014	25
Jedwali 4.1:	Idadi ya Wahalifu Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi na Mkoa , Tanzania Bara, 2013 na 2014	27
Jedwali 4.2:	Idadi wa Wafungwa Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Umri, Jinsi na Mkoa, Tanzania Bara, 2013	30
Jedwali 4.3:	Idadi ya Wafungwa Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani Kwa Umri, Jinsi na Mkoa , Tanzania Bara, 2014	30
Jedwali 4.4:	Idadi ya Wafungwa Warudiaji Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi, Mkoa na Urudiaji wa Kifungo, Tanzania Bara, 2013.....	32
Jedwali 4.5:	Idadi ya Wafungwa Warudiaji Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi, Mkoa na Urudiaji wa Kifungo, Tanzania Bara, 2014.....	33

Jedwali 4.6:	Idadi ya Wafungwa Watu Wazima Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi, Aina ya Kosa na Urefu wa Kifungo, Tanzania Bara, 2013	35
Jedwali 4.7:	Idadi ya Wafungwa Watu Wazima Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi, Aina ya Kosa na Urefu wa Kifungo, Tanzania Bara, 2014	36
Jedwali 4.8:	Idadi ya Wafungwa Vijana Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi, Aina ya kosa na Urefu wa Kifungo, Tanzania Bara, 2013	38
Jedwali 4.9:	Idadi ya Wafungwa Vijana Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi, Aina ya Kosa na Urefu wa Kifungo, Tanzania Bara, 2014	39
Jedwali 4.10:	Idadi ya Wafungwa Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Kushindwa Kulipa Faini kwa Mkoa na Urefu wa Kifungo, Tanzania Bara, 2013 na 2014.....	40
Jedwali 4.11:	Idadi ya Wahalifu Wanawake Wajawazito na Wenye Watoto Waliopokelewa Magerezani Toka Mahakamani Kulingana na Aina ya Kosa, Tanzania Bara, 2013 na 2014.....	42
Jedwali 4.12:	Idadi ya Mahabusu Watu Wazima Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi, Aina ya Kosa na Muda wa Kusubiri Hukumu, Tanzania Bara, 2013 na 2014	43
Jedwali 4.13:	Idadi ya Mahabusu Vijana Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi, Aina ya Kosa na Muda wa Kusubiri Hukumu, Tanzania Bara, 2013 na 2014.....	44
Jedwali 4.14:	Idadi ya Wafungwa Wasio Raia Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi na Nchi Walizotoka, Tanzania Bara, 2013 na 2014.	45
Jedwali 4.15:	Idadi ya Wafungwa Wasio Raia Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi na Aina ya Kosa, Tanzania Bara, 2013 na 2014	46
Jedwali 4.16:	Idadi ya Mahabusu Wasio Raia Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi na Nchi Walizotoka, Tanzania Bara, 2013 na 2014	47
Jedwali 4.17:	Idadi ya Mahabusu Wasio Raia Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi na Aina ya Kosa, Tanzania Bara, 2013 na 2014	48
Jedwali 5.1:	Idadi ya wahalifu Waliohamishwa kwa Jinsi na Mkoa, Tanzania Bara, 2013 na 2014	50
Jedwali 6.1:	Idadi ya Wahalifu Waliotoka Magerezani kwa Jinsi na Mkoa, Tanzania Bara, 2013	53

Jedwali 6.2:	Idadi ya Wahalifu Waliotoka Magerezani kwa Jinsi na Mkoa, Tanzania Bara, 2014	54
Jedwali 6.3:	Idadi Ya Wafungwa Walioachiwa kwenda Kutumikia Kifungo cha Nje kwa Jinsi na Mkoa , Tanzania Bara, 2013 na 2014.....	56
Jedwali 6.4:	Idadi ya Wafungwa Walioachiwa Baada ya Kulipa Faini kwa Urefu wa Kifungo na Mkoa , Tanzania Bara, 2013 na 2014.	58
Jedwali 6.5:	Idadi ya Wahalifu Waliotoroka Magerezani Chini ya Ulinzi Halali kwa Jinsi na Mkoa , Tanzania Bara, 2013 na 2014.....	59
Jedwali 6.6:	Idadi ya Wahalifu Waliofariki Magerezani kwa Jinsi na Mkoa, Tanzania Bara, 2013 na 2014.....	61
Jedwali 7. 1:	Idadi ya Wahalifu Waliopewa Adhabu Magerezani kwa Aina ya Adhabu na Mkoa , Tanzania Bara, 2013.....	63
Jedwali 7.2:	Idadi ya Wahalifu Waliopewa Adhabu Magerezani kwa Aina ya Adhabu na Mkoa, Tanzania Bara, 2014.....	64
Jedwali 8.1:	Idadi ya Mahabusu Waliohukumiwa Wakiwa Magerezani kwa Jinsi na Mkoa, Tanzania Bara, 2013 na 2014	66

Orodha ya Michoro

Mchoro 3.1:	Wahalifu Waliobaki Magerezani kwa Mkoa na Jinsi, Tanzania Bara, 2013 na 2014.....	7
Mchoro 3.2:	Wafungwa Waliobaki Magerezani kwa Umri, Tanzania Bara, 2013 na 2014.....	9
Mchoro 3.3:	Wafungwa wa Adhabu ya Kifo Waliobaki Magerezani na Hali ya Rufaa, Tanzania Bara, 2013 na 2014.....	12
Mchoro 3.4:	Wafungwa Watu Wazima na Vijana Waliobaki Magerezani, Tanzania Bara, 2013 na 2014	14
Mchoro 3.5:	Idadi ya Wafungwa Waliokuwepo Magerezani kwa Aina ya Kosa na Urefu wa Kifungo, Tanzania Bara, 2013 na 2014.	15
Mchoro 3.6:	Mahabusu Watu Wazima na Vijana Waliokuwepo Magerezani, Tanzania Bara, 2013 na 2014	17
Mchoro 3.7:	Idadi ya Mahabusu Watu Wazima Waliokuwepo Magerezani na Kusubiri Kesi kwa Aina ya Kosa na Muda Waliokaa Gerezani, Tanzania Bara, 2013 na 2014.....	18
Mchoro 3.8:	Idadi ya mahabusu vijana waliokuwepo magerezani na kusubiri kesi kwa aina ya kosa na muda waliokaa gerezani, Tanzania Bara 2013 na 2014.	19
Mchoro 3.9:	Idadi ya Wafungwa Wasio Raia Waliokuwepo Magerezani kwa Nchi Walizotoka, Tanzania Bara, 2013 na 2014	23
Mchoro 4.1:	Wahalifu Waliopokelewa MaGerezani Kutoka Mahakamani kwa Jinsi na Mkoa, Tanzania Bara, 2013 na 2014	28
Mchoro 4.2:	Wafungwa Warudiaji Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani, Tanzania Bara, 2013 na 2014.....	34
Mchoro 6.1:	Idadi ya Wahalifu Waliotoka Magerezani, Tanzania Bara, 2013 na 2014	55
Mchoro 6.2:	Wafungwa Walioachiwa kwenda Kutumikia Kifungo cha Nje kwa Jinsi na Mkoa , Tanzania Bara, 2013 na 2014.	57
Mchoro 6.3:	Wahalifu Waliotoroka Magerezani Chini ya Ulinzi Halali, Tanzania Bara, 2013 na 2014.	60

Majedwali Ambatanisho

Jedwali Na. 1:	Idadi ya Wahalifu Waliobaki Magerezani kwa Mkoa, Jinsi na Aina ya Uhalifu, Tanzania Bara, 2013	68
Jedwali Na. 2:	Idadi ya Wahalifu Waliobaki Magerezani kwa Mkoa, Jinsi na Aina ya Uhalifu Tanzania Bara, 2014	69
Jedwali Na. 3:	Idadi ya Wafungwa Waliobaki Magerezani kwa Mkoa, Umri na Jinsi, Tanzania Bara, 2013	70
Jedwali Na. 4:	Idadi ya Wafungwa Waliobaki Magerezani kwa Mkoa, Umri na Jinsi, Tanzania Bara, 2014	71
Jedwali Na. 5:	Idadi ya Wafungwa wa Adhabu ya Kifo Waliobaki Magerezani kwa Mkoa, Jinsi na Hali ya Rufaa, Tanzania Bara, 2013 na 2014	722
Jedwali Na. 6:	Idadi ya Wafungwa Watu Wazima waliokuwepo Magerezani kwa Aina ya Kosa na Urefu wa Kifungo, Tanzania Bara, 2013	73
Jedwali Na. 7:	Idadi ya Wafungwa Watu Wazima waliokuwepo Magerezani kwa Aina ya kosa na Urefu wa Kifungo, Tanzania Bara, 2014	74
Jedwali Na. 8:	Idadi ya Mahabusu Watu Wazima waliokuwepo Magerezani, Kusubiri Kesi kwa Aina ya kosa na Muda Waliokaa Gerezani, Tanzania Bara, 2013	75
Jedwali Na. 9:	Idadi ya Mahabusu Watu Wazima Waliokuwepo Magerezani, Kusubiri Kesi kwa Aina ya Kosa na Muda Waliokaa Gerezani, Tanzania Bara, 2014	76
Jedwali Na. 10:	Idadi ya Mahabusu Vijana Waliokuwepo Magerezani, Kusubiri Kesi kwa Aina ya Kosa na Muda Waliokaa Gerezani, Tanzania, Bara, 2013	77
Jedwali Na. 11:	Idadi ya Mahabusu Vijana Waliokuwepo Magereani, Kusubiri Kesi kwa Aina ya kosa na Muda Waliokaa Gerezani, Tanzania Bara, 2014.....	78
Jedwali Na. 12:	Idadi ya Wafungwa Wasio Raia Waliokuwepo Magerezani kwa Nchi Walizotoka na Aina yaKosa, Tanzania Bara, 2013	79
Jedwali Na. 13:	Idadi ya Wafungwa Wasio Raia Waliokuwepo Magerezani kwa Nchi Walizotoka na Aina yaKosa, Tanzania Bara, 2014	80
Jedwali Na. 14:	Idadi ya Mahabusu Wasio Raia Waliokuwepo Magerezani kwa Nchi Walizotoka na Aina ya Kosa, Tanzania Bara, 2013	81
Jedwali Na. 15:	Idadi ya Mahabusu Wasio Raia Waliokuwepo Magerezani kwa Nchi Walizotoka na Ainan ya Kosa, Tanzania Bara, 2014	82
Jedwali Na. 16:	Idadi ya Wahalifu Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Mkoa, Aina ya Muharifu na Jinsi, Tanzania Bara, 2013	84

Jedwali Na. 17: Idadi ya Wahalifu Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Mkoa, Aina ya Muharifu na Jinsi, Tanzania Bara, 2014	85
Jedwali Na.18: Idadi ya Wafungwa Wasio Raia Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Nchi Walizotoka na Aina ya Kosa, Tanzania Bara, 2013	86
Jedwali Na.19: Idadi ya Wafungwa Wasio Raia Waliopokelewa Magerezani Kutoka Mahakamani kwa Nchi Walizotoka na Aina ya Kosa, Tanzania Bara, 2014	87
Jedwali Na. 20: Idadi ya Mahabusu Wasio Raia Waliopokelewa Magerezani Toka Mahakamani kwa Nchi na Aina ya Kosa, Tanzania Bara, 2013.....	88
Jedwali Na. 21: Idadi ya Mahabusu Wasio Raia Waliopokelewa Magerezani Toka Mahakamani kwa Nchi na Aina ya Kosa, Tanzania Bara, 2014.....	89

MAANA YA VIFUPISHO

A/INSP	-	Mkaguzi Msaidizi wa Magereza
ASP	-	Mrakibu Msaidizi wa Magereza
CGP	-	Kamishna Jenerali wa Magereza
CP	-	Kamishna wa Magereza
CPL	-	Corporal
Dkt	-	Daktari
DPRK	-	Korea ya Kaskazini
DRC	-	Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo
EASTC	-	Chuo cha Takwimu cha Mashariki na Kusini mwa Afrika
Ke	-	Mwanamke
Me	-	Mwanaume
MKUKUTA	-	Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania
NBS	-	Ofisi ya Taifa ya Takwimu
O/I	-	Mkuu wa Gereza
RPO	-	Mkuu wa Magereza wa Mkoa
SP	-	Mrakibu wa Magereza
S/SGT	-	Sajin Taji
SGT	-	Sajenti
SSP	-	Mrakibu Mwandamizi wa Magereza
TPS	-	Jeshi la Magereza Tanzania
TSMP	-	Mpango Kabambe wa Kuboresha Takwimu Tanzania
TPF	-	Jeshi la Polisi Tanzania
UK	-	Uingereza
V	-	Vijana

DIBAJI



Dkt. Juma A. Malewa
Kamishna Jenerali wa Magereza

Jeshi la Magereza Tanzania Bara limeanza kutoa taarifa za kitakwimu za wafungwa na mahabusu waliopo magerezani kwa lengo la kuonesha idadi ya wahalifu waliopo, aina za wahalifu, hukumu, sifa na tabia za wahalifu hao.

Taarifa hizi zitaliwezesha Jeshi la Magereza kuboresha maeneo mbalimbali kama vile rasilimali watu, fedha na vifaa ili kuweza kupanga mikakati na mbinu mbalimbali zitakazotuwezesha kuwahifadhi na kuwarekebisha wafungwa waliopo magerezani mpaka watakapomaliza adhabu zao kwa mujibu wa sheria.

Hivi sasa Jeshi limebaini kuwa upo umuhimu wa kuboresha taarifa zake ili ziweze kwenda na wakati. Aidha, Jeshi la Magereza, kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) chini ya

Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Kuboresha na Kuimarisha Takwimu Tanzania, litakuwa linatoa taarifa mbalimbali za kitakwimu kutokana na data za ndani ya jeshi. Taarifa hizo, zitakuwa ni pamoja na za wafungwa na mahabusu kila baada ya kipindi cha robo mwaka ambazo baadae zitatumika kuandaa taarifa za mwaka mzima.

Taarifa hizi zitaonesha hali halisi itakayoliwezesha jeshi hili kujipanga vyema ili kuweza kuyafikia malengo yaliyowekwa, mojawapo likiwa ni kupunguza uhalifu kama ilivyoainishwa kwenye MKUKUTA.

Dkt* Juma A. Malewa,
Kamishna Jenerali wa Magereza,
Jeshi la Magereza Tanzania Bara,
DAR ES SALAAM.

SHUKRANI



Gaston K.Sanga
Kamishna wa Fedha na Utawala

Katika kukamilisha kazi hii, maofisa na askari magereza, wataalam kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu, pamoja na wadau mbalimbali wamehusika wakiongozwa na Mrakibu Mwandamizi wa Magereza Marco Kilumbo. Shukrani za kipekee ziwaendee Kamishna Jenerali wa Magereza Dkt.Juma A. Malewa, Mkuu wa Jeshi la Magereza nchini kwa kutoa maelekezo mbalimbali yaliyofanikisha kukamilika kwa kazi hii pamoja na kuwatia moyo watendaji wakati wa kuandaa taarifa hii na Dkt. Albina Chuwa, Mkurugenzi Mkuu, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ambaye kwa kupitia mradi wa TSMP aliwaruhusu wataalamu wake washirikiane na watendaji wa Magereza kufanikisha uandaaji wa Taarifa hii. Pia shukrani ziwaendee Kamishina Jenerali wa Magereza Mstaafu, John C. Minja na Kamishna wa Magereza Mstaafu, D.L. Chamulesile ambao kwa njia moja ama nyingine wameshiriki katika kutoa ushauri uliofanikisha kukamilika kwa kazi hii.

Aidha, shukrani za kipekee ziwaendee wataalamu walioshiriki katika uandishi wa ripoti hii; Valerian Tesha (NBS), SP-Emmanuel Pagali (TPS), ASP-Joseph Siwale (TPS), ASP-Deodatus Kazinja (TPS), S/SGT-Magdalena Landa (TPS), SGT-Ruth Mshiu (TPS), SGT-Consolatha Ragije (TPS), SGT-Desdery Mallya (TPS), CPL-Regnald Shaban (TPS), Ibrahimu Masanja (NBS), Eliaranya Lema (NBS), Clement Mwakanyamale (DPP) na SP-Andrew Mapunda (TPF).

Mwisho, shukrani za dhati ziwaendee wataalamu wote kutoka Chuo cha Takwimu cha Mashariki na Kusini mwa Afrika (EASTC) kwa mchango wao mkubwa katika kufanikisha taarifa hii na kuiweka katika kiwango kinachokubalika.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'K. Sanga'.

Gaston K. Sanga,
Kamishna wa Fedha na Utawala,
Makao Makuu ya Jeshi la Magereza.
DAR ES SALAAM.

MUHTASARI

Taarifa hii rasmi ya kitakwimu ni ya kwanza kutolewa na Jeshi la Magereza Tanzania Bara. Taarifa inahusu wafungwa na mahabusu waliokuwa magerezani katika kipindi cha mwaka 2013 na 2014. Pia inatoa ufafanuzi wa kina katika maeneo makuu sita (6). Eneo la kwanza ni wahalifu wote yaani wafungwa na mahabusu waliobaki magerezani mwishoni mwa mwaka 2013 na 2014, pili ni wafungwa na mahabusu waliopokelewa magerezani kutoka mahakamani kwa mwaka 2013 na 2014, tatu ni wafungwa na mahabusu waliohama na kuhamia katika magereza mengine kwa sababu mbalimbali. Eneo la nne linahusu wafungwa na mahabusu walioachiwa huru kwa sababu mbalimbali kama vile kumaliza adhabu zao kwa mujibu wa sheria. Eneo la tano linahusu mahabusu waliohukumiwa kifungo wakiwa magerezani na mwisho ni wafungwa na mahabusu waliopewa adhabu mbalimbali wakiwa magerezani.

Baada ya uchambuzi huo wa kina, hitimisho limetolewa kwa lengo la kuboresha hali ya magereza nchini.

SURA YA KWANZA

USULI

1.0 Utangulizi

Sura hii inaangalia Jiografia ya nchi na majukumu ya msingi ya Jeshi la Magereza Tanzania Bara. Takwimu zitakazotolewa na Jeshi la Magereza zitasaidia katika kupanga kwa makini mipango ya kuhakikisha uwepo wa rasilimali za kutosha, kusimamia na kutathmini matokeo ya utekelezaji wa mipango mbalimbali ya maendeleo. Rasilimali hizi zinahusisha watumishi (rasilimali watu), fedha na vitendea kazi, ofisi, vyombo vya usafiri na makazi bora ya askari na wafungwa. Kuhakikisha kuwapo rasilimali hizi ni muhimu katika kuweka mazingira bora ya utekelezaji wa mikakati na program mbalimbali za maendeleo katika Jeshi.

Aidha, kuna haja ya kuliboresha Jeshi la Magereza kuwa la kisasa zaidi kwa kutumia tekonolojia ya kisasa katika utekelezaji wa majukumu yake ya msingi kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Magereza Na. 34 ya Mwaka 1967. Hatua hii itachangia pia katika kuleta amani na utulivu nchini pamoja na kuendeleza na kudumisha usalama katika jamii kwa kuwahifadhi na kuwarekebisha wahalifu ili watokapo magerezani wawe raia wema watakaoshiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

1.1 Jiografia na Utawala

Tanzania ni jamhuri ya muungano wa nchi mbili, Tanganyika na Zanzibar. Nchi hizi ziliungana mwaka 1964. Tanzania ni miongoni mwa nchi tano (5) zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nchi nyingine ni Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi. Ipo kati ya latitudo 1^0 na 12^0 Kusini na na kati ya Longitudo 29^0 na 41^0 Mashariki mwa Greenwich. Ina eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 945,087. Nchi hii imepakana na Kenya na Uganda upande wa Kaskazini na Msumbiji upande wa Kusini. Mashariki imepakana na Bahari ya Hindi, upande wa Magharibi nchi za Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na upande wa Kusini Magharibi imepakana na nchi za Malawi na Zambia.

Tanzania ina maziwa makuu matatu; Victoria, Tanganyika na Nyasa. Ina vivutio vingi vya kitalii ukiwemo Mlima Kilimanjaro ambao ni mrefu kuliko yote Afrika na umefunikwa na theluji kwa kipindi chote cha mwaka pamoja na mbuga za wanyama, mambo ya kale na fukwe nzuri katika Pwani ya Tanzania Bara na katika visiwa vya Zanzibar.

Hali ya hewa ya Tanzania ni ya kitropiki kwa kipindi chote cha mwaka, ambapo maeneo mengi yana misimu miwili ya mvua za masika na vuli. Shughuli kubwa za kiuchumi ni kilimo, ufugaji,

utalii, uchimbaji wa madini, viwanda na huduma mbali mbali. Lugha kuu ya Taifa ni Kiswahili inayozungumzwa na takribani watu wote pamoja na kuwa Tanzania ina makabila zaidi ya 120.

Tangu mwaka 1992, Tanzania inafuata mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa. Dola ya Tanzania ina mihimili mitatu; Bunge, Serikali na Mahakama. Nchi hii ina mfumo wa Serikali mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kiutawala; Tanzania imegawanyika katika mikoa 30 ambapo 25 ipo Tanzania Bara na 5 ipo Tanzania Zanzibar.

1.2 Jeshi la Magereza

Jeshi la Magereza lilianzishwa rasmi tarehe 25 Agosti, 1931 baada ya mgawanyiko wa jeshi la Polisi na Magereza. Kwa sasa linaongozwa na Sheria ya Magereza Na. 34 ya mwaka 1967. Jeshi la Magereza limechangia kwa kiasi kikubwa katika kuleta amani na utulivu kwa kufanya kazi zake kikamilifu na kwa uadilifu mkubwa na kwa kuzingatia misingi ya haki za binadamu na utawala bora.

1.2.1 Majukumu ya Jeshi la Magereza

Majukumu ya Jeshi la Magereza kama yalivyoainishwa katika Sheria Na. 34 ya 1967 ni kuchangia katika kuleta amani na kuendeleza na kudumisha usalama katika jamii kwa kufanya yafuatayo:-

- i. Kuhifadhi wafungwa wa aina zote wanaowekwa chini ya ulinzi halali kisheria ndani ya magereza;
- ii. Kuandaa na kutekeleza programu za urekebishaji wa wafungwa na kuwafundisha wafungwa shughuli za uzalishaji na ujuzi mbalimbali kwa njia ya vitendo na ushauri;
- iii. Kuendesha shughuli za huduma za watuhumiwa (mahabusu) kwa mujibu wa sheria; na
- iv. Kutoa ushauri katika kuzuia na kudhibiti uhalifu na urekebishaji wa wahalifu.

Hivi sasa; Jeshi la Magereza lipo katika mchakato wa kufanya maboresho kwa lengo la kuwa ni Jeshi la kisasa linalofanya kazi zake kwa ufanisi, uwajibikaji na weledi wa hali ya juu ili kutimiza malengo yake liliyojiwekea kwa kiwango cha juu.

1.2.2 Takwimu za Jeshi la Magereza

Jeshi la Magereza lina Takwimu za aina tatu: Takwimu za kiutawala, Takwimu za uhalifu na Takwimu za uzalishaji mali. Takwimu za utawala zinahusu rasilimali watu, vifaa na fedha; takwimu za uhalifu zinahusu mchakato mzima wa kuwapokea, kuwahifadhi kwa ajili ya kutekeleza adhabu kama ni wafungwa au kuwapeleka mahakamani kwa ajili ya kusikiliza kesi zao kama ni mahabusu.

Vilevile kuwaachia huru wafungwa kwa mujibu wa sheria. Takwimu za uzalishaji mali zinahusu taarifa zote za uzalishaji katika miradi mbalimbali ya magereza ikiwemo kilimo, ufugaji na shughuli za viwanda vidogo vidogo. Takwimu hizi hulisaidia Jeshi la Magereza katika kupanga mipango yake ya kiutendaji na kimaendeleo. Aidha, sura ya 3 mpaka ya 8 ya ripoti hii zinatoa taarifa za kitakwimu za wafungwa na mahabusu katika magereza yetu kwa mwaka 2013 na 2014.

1.2.3 Kitengo cha Takwimu cha Jeshi la Magereza

Kitengo cha Takwimu cha Jeshi la Magereza kipo katika Kurugenzi ya Mipango. Kitengo hiki hupokea taarifa mbalimbali kutoka katika magereza, huzichambua, huzihifadhi, pamoja kuzitumia kuandaa taarifa za mwaka kwa kushirikiana na vitengo vingine.

SURA YA PILI

HALI YA MAGEREZA NCHINI

2.0 Utangulizi

Katika kipindi cha mwaka 2013 na 2014 hali ya ulinzi na usalama magerezani ilikuwa imara na hakukuwa na tukio lolote lisilo la kawaida. Pamoja na changamoto nyingi ambazo zilikwamisha utendaji katika baadhi ya majukumu ya kila siku, Jeshi la Magereza lilijitahidi sana kuyatatua na kufanya kazi zake kwa ufanisi wa kuridhisha.

2.1 Muhtasari wa Hali ya Magereza

Taarifa hii inajumuisha takwimu za mwaka 2013 na 2014, na ulinganisho wa takwimu hizi umefanyika ili kubaini mwenendo wa magereza Tanzania Bara. Ulinganifu huu unahusu idadi ya wahalifu waliobaki magerezani mwishoni mwa mwaka 2013 na 2014, wahalifu waliopokelewa katika miaka hiyo, wahalifu waliohamishwa kutoka gereza moja hadi jingine kwa sababu mbalimbali, wahalifu walioachiwa magerezani kwa sababu mbalimbali, wahalifu waliopewa adhabu kwa utovu wa nidhamu na mahabusu waliohukumiwa adhabu za vifungo wakiwa magerezani.

SURA YA TATU

TAKWIMU ZA WAHALIFU WALIOKUWEPO MAGEREZANI

3.0 Utangulizi

Taarifa hii ni ya wahalifu waliokuwepo magerezani mwishoni mwa mwaka 2013 na 2014. Katika magereza yote kulikuwa na wahalifu 33,807 kwa mwaka 2013 na 33,517 mwaka 2014 (Jedwali 3.1 na Mchoro 3.1). Idadi ya mwaka 2014 ilikuwa pungufu kwa wahalifu 290 ambao ni sawa na asilimia 0.9 ikilinganishwa na idadi ya mwaka 2013.

Kati ya wahalifu waliokuwepo magerezani tarehe 31.12.2013, mahabusu walikuwa 17,214 (Jedwali Ambatanisho 1) sawa na asilimia 50.9 na wafungwa 16,593 sawa na asilimia 49.1. Mwaka 2014 mahabusu walikuwa 16,926 sawa na asilimia 50.5 ambapo wafungwa walikuwa 16,591 sawa na asilimia 49.5.

3.1 Takwimu za Wahalifu kwa Mikoa na Jinsi

Takwimu zinaonesha kuwa mwaka 2013 wahalifu wanaume walikuwa 32,215 sawa na asilimia 95.3, wanawake 1,243 sawa na asilimia 3.7 ambapo wahalifu vijana walikuwa 349 sawa na asilimia 1.0. Ambapo, mwaka 2014 wanaume wahalifu walikuwa 31,930 sawa na asilimia 95.2, wanawake 1,326 sawa na asilimia 4.0 na vijana 261 sawa na asilimia 0.8.

Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na wahalifu wengi kuliko mikoa mingine kwa miaka yote miwili ambapo mwaka 2013 walikuwa 4,144 na mwaka 2014 walikuwa 4,360. Mkoa wa Ruvuma ulikuwa na wahalifu wachache (529) mwaka 2013 ., ambapo mwaka 2014 Mkoa wa Lindi ulikuwa na wahalifu wachache (410).


Pamoja na kuwa na wahalifu 33,807 mwaka 2013 na 33,517 mwaka 2014, uwezo wa magereza nchini ni kuhifadhi wahalifu 29,552 tu. Kwa hiyo idadi ya wahalifu ya mwaka 2013 na 2014 ni zaidi ya idadi inayoruhusiwa kisheria.

Jedwali 3.1: Idadi ya Wahalifu Waliobaki Magerezani kwa Mkoa na Jinsi, Tanzania Bara, 2013 na 2014

Mkoa	2013				2014			
	Watu Wazima		V	Jumla	Watu Wazima		V	Jumla
	Me	Ke			Me	Ke		
Arusha	1,156	32	0	1,188	1,191	51	1	1,243
Dar es Salaam	4,015	113	16	4,144	4,197	146	17	4,360
Dodoma	1,826	56	18	1,900	1,656	50	16	1,722
Iringa	1,229	64	3	1,296	1,080	56	14	1,150
Kagera	1,848	163	4	2,015	2,150	95	6	2,251
Kigoma	1,403	89	79	1,571	1,147	72	10	1,229
Kilimanjaro	1,429	66	10	1,505	1,447	62	0	1,509
Lindi	575	11	5	591	400	10	0	410
Manyara	912	37	0	949	982	35	0	1,017
Mara	1,743	47	19	1,809	1,923	106	19	2,048
Mbeya	2,072	73	8	2,153	1,773	74	1	1,848
Morogoro	1,588	69	42	1,699	1,604	75	40	1,719
Mtwara	812	25	0	837	743	24	1	768
Mwanza	3,317	159	108	3,584	3,158	137	82	3,377
Pwani	823	14	0	837	925	15	0	940
Ruvuma	510	18	1	529	680	23	0	703
Rukwa	892	32	6	930	891	40	14	945
Singida	855	47	24	926	813	55	2	870
Shinyanga	1,711	68	6	1,785	1,876	85	24	1,985
Tabora	1,984	34	0	2,018	2,087	43	0	2,130
Tanga	1,515	26	0	1,541	1,207	72	14	1,293
Jumla	32,215	1,243	349	33,807	31,930	1,326	261	33,517

Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

Mchoro 3.1: Wahalifu Waliobaki Magerezani kwa Mkoa na Jinsi, Tanzania Bara, 2013 na 2014



Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

3.2 Wafungwa Waliobaki Magerezani kwa Mkoa na Umri

Wafungwa wengi waliobaki magerezani kwa mwaka 2013 na 2014 ni wale wenye umri kuanzia 15 hadi miaka 50 ambapo mwaka 2013 walikuwa 14,219 sawa na asilimia 85.7 na mwaka 2014 walikuwa 14,518 sawa na asilimia 87.5 (Jedwali 3.2 na Mchoro 3.2).


Wafungwa wa umri huu ndiyo hasa nguvu kazi ya taifa letu hivyo hakuna budi juhudi kubwa . zifanyike kuwarekebisha ili watakapotoka wawe raia wema watakaojenga taifa lao.

Jedwali 3.2: Idadi ya Wafungwa Waliobaki Magerezani kwa Mkoa na Umri, Tanzania Bara, 2013 na 2014

Mkoa	2013					2014				
	Miaka 15 - 20	Miaka 21 - 25	Miaka 26 - 50	Zaidi ya miaka 50	Jumla	Miaka 15 - 20	Miaka 21 - 25	Miaka 26 - 50	Zaidi ya miaka 50	Jumla
Arusha	71	117	105	210	503	101	153	119	94	467
Dar es Salaam	641	163	816	310	1,930	629	134	729	375	1,867
Dodoma	170	194	637	107	1,108	156	198	533	95	982
Iringa	122	150	100	54	426	147	204	94	23	468
Kagera	163	244	450	130	987	172	196	455	265	1,088
Kigoma	213	222	328	95	858	145	131	393	32	701
Kilimanjaro	79	345	224	38	686	89	437	315	26	867
Lindi	96	74	174	22	366	42	30	119	21	212
Manyara	61	75	204	104	444	33	206	253	35	527
Mara	205	89	206	141	641	320	60	319	123	822
Mbeya	100	191	324	446	1,061	126	151	349	247	873
Morogoro	218	276	383	100	977	166	356	369	101	992
Mtwara	142	51	192	41	426	144	51	220	55	470
Mwanza	521	367	687	222	1,797	429	333	686	212	1,660
Pwani	82	155	162	19	418	100	305	171	54	630
Ruvuma	54	106	101	21	282	131	134	145	33	443
Rukwa	102	51	312	24	489	69	112	245	24	450
Singida	56	118	173	35	382	45	98	154	19	316
Shinyanga	169	287	221	60	737	200	195	304	75	774
Tabora	274	221	641	83	1,219	293	396	524	88	1,301
Tanga	81	327	336	112	856	67	292	246	76	681
Jumla	3,620	3,823	6,776	2,374	16,593	3,604	4,172	6,742	2,073	16,591

Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

Mchoro 3.2: Wafungwa Waliobaki Magerezani kwa Umri, Tanzania Bara, 2013 na 2014



Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

3.3 Wafungwa Waliobaki Magerezani kwa Mkoa, Jinsi na Tabia

Kitabia, kuna aina mbili za wafungwa magerezani, kwanza ni wafungwa wenye tabia nzuri (*Star*). Hawa ni wafungwa waliohukumiwa kifungo magerezani kwa mara ya kwanza au kwa mara ya pili ambao historia ya uhalifu wao, tabia zao na aina ya makosa ya nyuma waliyotenda wanaonekana wanafaa kwa urekebishaji na mafunzo. Kundi la pili ni wafungwa wa kawaida (*Ordinary*) ambao ni wale waliokosa sifa ya kuwa *Star*.

Walikuwepo wafungwa 16,593 magerezani mwaka 2013 na kati yao 10,539 sawa na asilimia 63.5 walikuwa wafungwa wenye tabia nzuri (*star*) na 6,054 sawa na asilimia 36.5 walikuwa wafungwa wa kawaida (*ordinary*). Kwa mwaka 2014 wafungwa walikuwa 16,591 na kati yao 10,958 sawa na asilimia 66.0 walikuwa wafungwa wenye tabia nzuri (*star*) na 5,633 walikuwa wafungwa wa kawaida (*ordinary*) sawa na asilimia 34.0 kama Jedwali 3.3 linavyoonesha.

Jedwali 3.3: Idadi ya Wafungwa Waliobaki Magerezani kwa Mkoa, Jinsi na Tabia, Tanzania Bara, 2013 na 2014

Mkoa	2013									2014								
	Tabia nzuri				Tabia ya kawaida				Jumla Kuu	Tabia nzuri				Tabia ya kawaida				Jumla Kuu
	Me	Ke	V	Jumla	Me	Ke	V	Jumla		Me	Ke	V	Jumla	M	Ke	V	Jumla	
Arusha	329	5	0	334	166	3	0	169	503	111	3	0	114	346	6	1	353	467
Dar es Salaam	509	0	0	509	1,391	29	1	1,421	1,930	404	0	0	404	1,437	26	0	1,463	1,867
Dodoma	415	9	8	432	663	13	0	676	1,108	349	18	5	372	608	2	0	610	982
Iringa	298	14	0	312	114	0	0	114	426	377	11	0	388	80	0	0	80	468
Kagera	663	29	1	693	294	0	0	294	987	853	23	3	879	209	0	0	209	1,088
Kigoma	601	26	20	647	211	0	0	211	858	490	17	8	515	185	1	0	186	701
Kilimanjaro	603	15	0	618	67	1	0	68	686	768	13	0	781	82	4	0	86	867
Lindi	271	3	5	279	86	1	0	87	366	154	2	0	156	56	0	0	56	212
Manyara	376	11	0	387	57	0	0	57	444	477	10	0	487	40	0	0	40	527
Mara	457	7	4	468	171	2	0	173	641	677	14	5	696	121	5	0	126	822
Mbeya	723	19	2	744	312	1	4	317	1,061	697	18	0	715	155	3	0	158	873
Morogoro	439	4	24	467	473	30	7	510	977	589	12	13	614	330	30	18	378	992
Mtwara	298	6	0	304	118	4	0	122	426	309	6	1	316	154	0	0	154	470
Mwanza	1,056	38	6	1,100	692	4	1	697	1,797	905	24	25	954	703	3	0	706	1,660
Pwani	238	4	0	242	175	1	0	176	418	340	3	0	343	287	0	0	287	630
Ruvuma	209	1	0	210	72	0	0	72	282	302	8	0	310	133	0	0	133	443
Rukwa	373	6	2	381	108	0	0	108	489	357	8	9	374	76	0	0	76	450
Singida	306	11	3	320	61	1	0	62	378	166	10	0	176	140	0	0	140	316
Shinyanga	438	20	2	460	276	0	1	277	737	551	29	0	580	190	4	0	194	774
Tabora	1,097	4	0	1,101	112	6	0	118	1,219	1,167	9	0	1,176	125	0	0	125	1,301
Tanga	524	7	0	531	325	0	0	325	856	585	23	0	608	72	1	0	73	681
Jumla	10,223	239	77	10,539	5,944	96	14	6,054	16,593	10,628	261	69	10,958	5,529	85	19	5,633	16,591

Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

3.4 Wafungwa wa Adhabu ya Kifo Waliobaki Magerezani kwa Mkoa na Hali ya Rufaa.

Jedwali 3.4 na Mchoro 3.3 vinaonesha idadi ya wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kifo waliokuwepo magerezani. Mwaka 2013 walikuwepo wafungwa 391, ikilinganishwa na wafungwa 410 kwa mwaka 2014, ikiwa ni ongezeko la wafungwa 19 sawa na asilimia 4.9.


Jumla ya wafungwa 391 wa mwaka 2013 walikata rufaa Mahakama ya Rufaa ya Tanzania. Kati ya hao, 233 sawa na asilimia 59.6 rufaa zao zilikataliwa na wafungwa 158 sawa na asilimia 40.4 waliendelea kusubiri kusikilizwa kwa rufaa zao. Mwaka 2014 wafungwa waliokata rufaa na rufaa zao zikakataliwa walikuwa 212 sawa na asilimia 51.7, ambapo 198 sawa na asilimia 48.3 waliendelea kusubiri kusikilizwa kwa rufaa zao. Wafungwa ambao rufaa zao zilikataliwa wanasubiri utekelezaji wa hukumu ya kifo. (Jedwali Ambatanisho 5).

Jedwali 3.4: Idadi ya wafungwa wa Adhabu ya Kifo Waliobaki Magerezani kwa Mkoa na Hali ya Rufaa, Tanzania Bara, 2013 na 2014

Mkoa	2013			2014		
	Rufaa zilizokataliwa	Rufaa ambazo hazijasikilizwa	Jumla	Rufaa zilizokataliwa	Rufaa ambazo hazijasikilizwa	Jumla
Arusha	6	10	16	6	8	14
Dar es Salaam	40	13	53	40	37	77
Dodoma	60	49	109	56	45	101
Iringa	0	0	0	0	0	0
Kagera	0	0	0	0	0	0
Kigoma	0	0	0	0	0	0
Kilimanjaro	0	2	2	0	2	2
Lindi	1	6	7	1	1	2
Manyara	0	1	1	0	0	0
Mara	0	0	0	0	0	0
Mbeya	6	25	31	8	18	26
Morogoro	0	0	0	0	0	0
Mtwara	6	3	9	5	6	11
Mwanza	29	32	61	28	50	78
Pwani	0	0	0	0	0	0
Ruvuma	0	0	0	0	0	0
Rukwa	0	0	0	0	0	0
Singida	0	0	0	0	0	0
Shinyanga	0	0	0	0	2	2
Tabora	25	8	33	29	19	48
Tanga	60	9	69	39	10	49
Jumla	233	158	391	212	198	410

Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

Mchoro 3.3: Wafungwa wa Adhabu ya Kifo Waliobaki Magerezani na Hali ya Rufaa, Tanzania Bara, 2013 na 2014



Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

3.5 Wafungwa Watu Wazima na Vijana Waliobaki Magerezani kwa Jinsi na Aina ya Kosa

Wafungwa watu wazima waliokuwepo magerezani mwaka 2013 walikuwa 16,502 wakilinganishwa na 16,503 wa mwaka 2014 ambao ni zaidi ya mfungwa 1 tu. Mwaka 2013 kosa liliofanywa na wafungwa wengi kuliko makosa mengine lilikuwa wizi ambalo lilikuwa na wafungwa 3,883. Lakini, mwaka 2014 kosa la kuvunja nyumba ndilo lililokuwa na wafungwa wengi kuliko mengine ambapo lilikuwa na wafungwa 2,476.


Aidha mwaka 2013 jumla ya wafungwa vijana waliokuwepo katika magereza yote Tanzania Bara walikuwa 91, ikilinganishwa na wafungwa 88 wa mwaka 2014, ambao ni pungufu kwa wafungwa 3 sawa na asilimia 3.3. Ingawa mwaka 2013, kosa lililokuwa na wafungwa wengi kuliko mengine ni kuvunja nyumba, kwa mwaka 2013 na 2014 wafungwa wengi vijana waliokuwepo magerezani walihukumikiwa kwa makosa ya wizi (Jedwali 3.5 na Mchoro 3.4).

Jedwali 3.5: Idadi ya Wafungwa Watu Wazima na Vijana Waliobaki Magerezani kwa Jinsi na Aina ya Kosa, Tanzania Bara, 2013 na 2014

Aina ya Kosa	2013						2014					
	Watu Wazima			Vijana			Watu Wazima			Vijana		
	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Mauaji	561	22	583	7	0	7	621	21	642	0	0	0
Mauaji (adhabu ya kifo kuwa kifungo)	120	0	120	0	0	0	154	1	155	0	0	0
Kuua bila kukusudia	821	45	866	1	0	1	1,212	50	1,262	8	0	8
KujaribuKujaribu kuua	167	8	175	5	1	6	182	6	188	5	0	5
Unyang'anyi	2,363	8	2,371	13	0	13	2,269	19	2,288	10	0	10
Wizi	3,794	89	3,883	14	1	15	2,223	59	2,282	16	1	17
Kuvunja nyumba	2,178	32	2,210	16	0	16	2,441	35	2,476	11	0	11
Kupatikana na dawa za kulevya	530	5	535	7	0	0	448	20	468	4	0	4
Kupatikana na nyara za serikali	374	1	375	1	0	1	562	4	566	4	0	4
Makosa ya kujamiiiana	909	5	914	4	1	5	1,785	17	1,802	8	1	9
Kupatikana na silaha na risasi	449	10	459	3	0	3	693	12	705	4	0	4
Kujeruhi	1,030	45	1,075	5	0	5	1,268	41	1,309	7	0	7
Kuchoma nyumba moto	119	0	119	0	0	0	185	15	200	2	0	2
Makosa ya rushwa	23	2	25	0	0	0	19	2	21	0	0	0
Kupatikana na pombe ya moshi (gongo)	165	10	175	0	0	0	394	21	415	2	0	2
Uzembe na uzururaji	153	2	155	0	0	0	191	0	191	0	0	0
Makosa mengineyo	2,411	51	2,462	11	1	12	1,510	23	1,533	5	0	5
Jumla	16,167	335	16,502	87	4	91	16,157	346	16,503	86	2	88

Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

Mchoro 3.4: Wafungwa Watu Wazima na Vijana Waliobaki Magerezani, Tanzania Bara, 2013 na 2014



Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

3.6 Wafungwa Waliokuwepo Magerezani kwa Jinsi, Aina ya Kosa na Urefu wa Kifungo


Jedwali 3.6 na Mchoro 3.5 vinaonesha idadi ya wafungwa waliokuwepo magerezani Tanzania Bara kwa aina ya kosa, jinsi na urefu wa kifungo kwa mwaka 2013 na 2014. Kwa miaka yote miwili takwimu zinaonesha kwamba kifungo chenye wafungwa wengi kuliko vingine ni cha zaidi ya mwaka mmoja hadi mitatu. Mwaka 2013 wafungwa walikuwa 3,268 sawa na asilimia 19.8, na mwaka 2014 walikuwa 2,606 sawa na asilimia 15.8. Aidha, kosa lililokuwa na wafungwa wengi kuliko makosa mengine lilikuwa wizi ambalo mwaka 2013 lilikuwa na wafungwa 3,883 sawa na asilimia 23.5 na mwaka 2014 walikuwa 4,413 sawa na asilimia 26.7 (Majedwali Ambatanisho 6 na 7).

Jedwali 3.6: Idadi ya Wafungwa Watu Wazima Waliokuwepo Magerezani kwa Jinsi na Urefu wa Kifungo, Tanzania Bara, 2013 na 2014

Urefu wa kifungo	2013			2014		
	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Hadi miezi 6	1,536	40	1,576	1,834	83	1,917
Zaidi ya miezi 6 hadi mwaka 1	2,568	107	2,675	2,293	54	2,347
Zaidi ya mwaka 1 hadi miaka 3	3,185	83	3,268	2,534	72	2,606
Zaidi ya miaka 3 hadi miaka 5	2,444	41	2,485	2,340	39	2,379
Zaidi ya miaka 5 hadi miaka 10	1,983	25	2,008	1,667	30	1,697
Zaidi ya miaka 10 hadi miaka 15	1,237	8	1,245	1,117	15	1,132
Zaidi ya miaka 15 hadi miaka 20	684	7	691	700	12	712
Zaidi ya miaka 20 hadi miaka 30	1,177	3	1,180	1,520	11	1,531
Zaidi ya miaka 30	526	0	526	1,001	1	1,002
Kifungo cha maisha	453	4	457	756	14	769
Adhabu ya kifo	374	17	391	395	15	410
Jumla	16,167	335	16,502	16,157	346	16,503

Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

Mchoro 3.5: Idadi ya Wafungwa Waliokuwepo Magerezani kwa Aina ya Kosa na Urefu wa Kifungo, Tanzania Bara, 2013 na 2014.



Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

3.7 Mahabusu Watu Wazima na Vijana Waliokuwepo Magerezani Kusubiri Kesi kwa Jinsi, Aina ya Kosa na Muda Waliokaa Gerezani


Mwaka 2013 walikuwepo mahabusu 17,214 waliobaki magerezani kusubiri hukumu, kati yao watu wazima walikuwa 16,956 na vijana walikuwa 258. Mwaka 2014 mahabusu walipungua na kufikia 16,926 ambapo watu wazima walikuwa 16,753 na vijana walikuwa 173. Idadi ya mahabusu watu wazima iliyopungua ni 288 ambao ni asilimia 1.7. Kwa miaka yote miwili kosa liliokuwa na mahabusu wengi kuliko mengine ni mauaji. Kosa hili lilikuwa na mahabusu 4,693 mwaka 2013 na 3,829 mwaka 2014 (Jedwali 3.7). Makosa haya ya mauaji yamewafanya baadhi ya mahabusu kusubiri kwa zaidi ya miaka kumi (10) kufikia hatma ya mashauri yao (Jedwali Ambatanisho 8 na 9; Mchoro 3.7.

Jedwali 3.7: Idadi ya Mahabusu Waliokuwepo Magerezani kwa Jinsi na Aina ya Kosa, Tanzania Bara, 2013 na 2014

Aina ya Kosa	2013						2014					
	Watu wazima			Vijana			Watu wazima			Vijana		
	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Mauaji	4,323	319	4,642	45	6	51	3,450	339	3,789	31	9	40
Mauaji (adhabu ya kifo kuwa kifungo)	0	0	0	0	0	0	0	0	0	3	0	3
Kuua bila kukusudia	903	27	930	5	1	6	854	14	868	5	1	6
Kujaribu kuua	1,099	91	1,190	8	0	8	1,457	114	1,571	21	0	21
Unyang'anyi	2,186	62	2,248	29	1	30	1,991	23	2,014	0	0	0
Wizi	1,667	105	1,772	30	4	34	1,826	128	1,954	23	2	25
Kuvunja nyumba	877	28	905	19	0	19	1,268	33	1,301	0	1	3
Kupatikana na dawa za kulevya	503	12	515	11	1	12	781	21	802	6	0	6
Kupatikana na nyara za Serikali	417	18	435	17	0	17	492	4	496	3	0	3
Makosa ya kujamiiana	848	26	874	13	1	14	626	18	644	20	0	20
Kupatikana na bunduki au risasi	135	6	141	2	0	2	192	6	198	1	0	1
Kujeruhi	545	36	581	8	0	8	648	32	680	3	0	3
Kuchoma moto nyumba	91	26	117	3	1	4	204	5	209	4	0	4
Makosa ya rushwa	89	15	104	1	1	2	97	0	97	1	0	1
Kupatikana na pombe ya moshi	789	109	898	31	1	32	864	62	926	26	0	24
Uzembe na uzururaji	149	6	155	4	1	5	36	2	38	0	0	0
Makosa mengineyo	1,427	22	1,449	14	0	14	987	179	1,166	11	2	13
Jumla	16,048	908	16,956	240	18	258	16,048	908	16,753	158	15	173


Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

Mchoro 3.6: Mahabusu Watu Wazima na Vijana Waliokuwepo Magerezani, Tanzania Bara, 2013 na 2014




Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

Mchoro 3.7: Idadi ya Mahabusu Watu Wazima Waliokuwepo Magerezani na Kusubiri Kesi kwa Aina ya Kosa na Muda Waliokaa Gerezani, Tanzania Bara, 2013 na 2014



Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

Mchoro 3.8: Idadi ya mahabusu vijana waliokuwepo magerezani na kusubiri kesi kwa aina ya kosa na muda waliokaa gerezani, Tanzania Bara 2013 na 2014.



Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

3.8 Wahalifu Wenye Ugonjwa wa Akili Waliobaki Magerezani

Hawa ni watu wenye ugonjwa wa akili ambao wanaweza wakawa wamefanya kosa/uhalifu au kutofanya kosa lakini kuwepo kwao uraiani, ni hatari kwao wenyewe na kwa jamii inayowazunguka. Mwaka 2013 kulikuwa na wahalifu 5 wenye ugonjwa wa akili, kati ya yao mmoja alikuwa Mkoa wa Dodoma na 4 walikuwa Tabora. Aidha, mwaka 2014 kulikuwa na mahabusu mmoja tu aliyekuwa mgonjwa wa akili na alikuwa mkoani Dodoma.

3.9 Wahalifu wanawake wajawazito na wenye watoto

Mwaka 2013 walikuwapo wafungwa wajawazito 9 na wafungwa wenye watoto 16, ambao walikuwa na watoto 18. Aidha, mwaka huo huo mahabusu wajawazito walikuwa 30, mahabusu wenye watoto 82 ambao walikuwa na watoto 87. Mwaka 2014 walikuwepo wafungwa wajawazito 6 na wafungwa 10 wenye watoto 10. Kwa mwaka huo huo mahabusu wajawazito walikuwa 27, mahabusu wenye watoto 78 wakiwa na watoto 85. Sababu kubwa zilizowaweka wahalifu wa kike gerezani ni makosa ya mauaji na wizi (Jedwali 3.8).

Jedwali 3.8 Idadi ya Wahalifu Wanawake Wajawazito na Wenye Watoto kwa Aina ya Kosa, Tanzania Bara, 2013 na 2014

Aina ya Kosa	2013						2014					
	Wafungwa			Mahabusu			Wafungwa			Mahabusu		
	Wajawazito	Wenye watoto		Wajawazito	Wenye watoto		Wajawazito	Wenye watoto		Wajawazito	Wenye watoto	
		Idadi ya wafungwa	Idadi ya watoto		Idadi ya mahabusu	Idadi ya watoto		Idadi ya wafungwa	Idadi ya watoto		Idadi ya mahabusu	Idadi ya watoto
Mauaji	0	5	5	11	40	40	1	1	1	10	53	58
Mauaji (adhabu ya kifo kuwa kifungo)	0	0	0	3	5	5	0	0	0	1	3	4
Kua bila kukusudia	0	0	0	2	0	0	0	1	1	2	1	1
Kujaribu kuaa	0	0	0	0	1	1	0	1	1	1	2	2
Unyang'anyi	1	0	0	0	0	0	0	0	0	1	1	1
Wizi	3	5	6	4	6	6	0	2	2	3	4	4
Kuvunja na kuiba	0	0	0	0	2	3	0	0	0	2	2	2
Kupatikana na dawa za Kulevya	0	1	1	0	1	1	1	0	0	1	3	3
Kupatikana na nyara za serikali	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Kujamiiana	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Kupatikana na silaha/risasi	1	1	1	0	2	2	0	1	1	0	0	0
Kujeruhi	1	2	2	4	5	6	2	2	2	0	4	4
Kuchoma nyumba moto	0	0	0	0	0	0	1	1	1	0	0	0
Rushwa	0	0	0	0	1	1	0	0	0	0	0	0
Kupatikana na pombe haramu (gongo)	0	1	1	0	1	1	0	0	0	0	0	0
Uzururaji	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Makosa mengineyo	3	1	2	6	18	21	1	1	1	6	5	6
Jumla	9	16	18	30	82	87	6	10	10	27	78	85

Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

3.10 Wafungwa Wasio Raia Waliokuwepo Magerezani, kwa Jinsi, Aina ya Kosa na Nchi Walizotoka

Wafungwa wasio raia wa Tanzania waliokuwapo magerezani mwaka 2013 ni 1,359, wakati mwaka 2014 walikuwa 873 ambao ni pungufu kwa wafungwa 486 sawa na asilimia 35.8. Wengi wa wafungwa hao walitoka katika nchi za Ethiopia na Burundi ambapo kwa mwaka 2013 wafungwa wengi walitoka Ethiopia ambapo walikuwa 660 sawa na asilimia 48.6. Mwaka 2014 wafungwa wengi walitoka Burundi idadi yao ilikuwa 460 sawa na asilimia 52.7 (Jedwali 3.9, Majedwali Ambatanisho 12 na 13 na Michoro 3.9).


Aidha, kwa miaka yote miwili wafungwa wengi wasio raia wa Tanzania walikuwa wanaume ambapo mwaka 2013 walikuwa 1,339 (asilimia 98.5) kulinganisha na wafungwa wa kike 20 (asilimia 1.5) na mwaka 2014 wanaume walikuwa 868 (asilimia 99.4) na wanawake walikuwa 5 (asilimia 0.6). Mwaka 2013 na 2014 kulionekana kulikuwa na wafungwa wengi wa makosa mengineyo kama vile kuingia nchini bila kibali, kupigana, kutukana na n.k (Jedwali 3.9).

Jedwali 3.9: Idadi ya Wafungwa Wasio Raia Waliokuwepo Magerezani kwa Jinsi na Aina ya Kosa Tanzania Bara, 2013 na 2014

Aina ya Kosa	2013			2014		
	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Mauaji	43	0	43	8	0	8
Mauaji (adhabu ya kifo kuwa kifungo)	1	0	1	0	0	0
Kuua bila kukusudia	10	3	13	14	0	14
Kujaribu kuua	0	0	0	0	0	0
Unyang'anyi	62	0	62	67	0	67
Wizi	56	5	61	67	0	67
Kuvunja nyumba	19	1	20	16	0	16
Kupatikana na madawa ya kulevya	5	0	5	3	0	3
Kupatikana na nyara za serikali	6	0	6	3	0	3
Makosa ya kujamiiana	40	0	40	23	0	23
Kupatikana na bunduki na risasi	37	0	37	20	0	20
Kujeruhi	14	3	17	8	0	8
Kuchoma moto nyumba	0	0	0	3	1	4
Makosa ya rushwa	0	0	0	0	0	0
Kupatikana na pombe ya moshi	0	0	0	2	0	2
Uzembe na uzururaji	0	0	0	0	0	0
Makosa mengine	1,046	8	1,054	634	4	638
Jumla	1,339	20	1,359	868	5	873

Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

Mchoro 3.9: Idadi ya Wafungwa Wasio Raia Waliokuwepo Magerezani kwa Nchi Walizotoka, Tanzania Bara, 2013 na 2014



Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

3.11 Mahabusu Wasio Raia Waliokuwepo Magerezani kwa Aina ya Kosa na Jinsi

Mwaka 2013 jumla ya mahabusu 841 wasio raia wa Tanzania walikuwepo magerezani. Wakati mwaka 2014 walikuwa 583 wakiwa ni pungufu kwa mahabusu 258 sawa na asilimia 30.7 wakilinganishwa na wale wa 2013. Mahabusu 280 sawa na asilimia 33.3 waliokuwepo magerezani mwaka 2013 ni raia wa Burundi Jedwali 3.11 na 3.12). Mwaka 2014 mahabusu walikuwa 243 (asilimia 41.7), wengi wao wakiwa ni watuhumiwa wa makosa mengineyo (kama vile kuingia nchini bila kibali, kupigana, kutukana na n.k).

Kwa miaka yote miwili, wengi wa mahabusu wasio raia wa Tanzania walikuwa wanaume. Mwaka 2013 wanaume walikuwa 797 (asilimia 94.8) kulinganisha na mahabusu wa kike walikuwa 44 (asilimia 5.2) ambapo mwaka 2014 wanaume walikuwa 545 (asilimia 93.5) na mahabusu wanawake walikuwa 38 (asilimia 6.5) Jedwali 3.10.

Jedwali 3.10: Idadi ya Mahabusu Wasio Raia Waliokuwepo Magerezani kwa Aina ya Kosa na Jinsi Tanzania Bara, 2013 na 2014

Aina ya Kosa	2013			2014		
	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
Mauaji	107	5	112	74	10	84
Mauaji (adhabu ya kifo kuwa kifungo)	0	0	0	0	0	0
Kua bila kukusudia	3	0	3	0	0	0
Kujaribu kua	3	0	3	12	0	12
Unyang'anyi	11	0	11	49	0	49
Wizi	79	4	83	41	4	45
Kuvunja nyumba	97	1	98	11	0	11
Kupatikana na madawa ya kulevya	37	9	46	70	0	70
Kupatikana na nyara za serikali	15	0	15	8	0	8
Makosa ya kujamiiana	37	0	37	13	0	13
Kupatikana na silaha na risasi	5	0	5	6	0	6
Kujeruhi	16	6	22	30	8	38
Kuchoma moto nyumba	0	0	0	0	0	0
Makosa ya rushwa	0	0	0	0	0	0
Kupatikana na pombe ya moshi	0	0	0	4	0	4
Uzembe na uzururaji	6	0	6	0	0	0
Makosa mengineyo	381	19	400	227	16	243
Jumla	797	44	841	545	38	583

Chanzo: Jeshi la Magereza Tanzania Bara

Jedwali 3.11: Idadi ya Mahabusu Wasio Raia Waliokuwepo Magerezani kwa Jinsi na Nchi Walizotoka, Tanzania Bara, 2013 na 2014

2013				2014			
Nchi Walizotoka	Me	Ke	Jumla	Nchi Walizotoka	Me	Ke	Jumla
Bulgaria	1	-	1	Burundi	227	17	244
Burundi	265	15	280	China	3	-	3
Cameroon	-	1	1	Colombia	1	-	1
China	3	-	3	Congo	20	-	20
Congo	2	-	2	DRC	3	-	3
DRC	4	-	4	Ethiopia	26	-	26
Ethiopia	222	-	222	Ujerumani	1	-	1
Ghana	1	-	1	Ghana	1	-	1
Ugiriki	1	-	1	Ugiriki	1	-	1
Guinea	1	-	1	Guinea	1	-	1
